



Wapendwa Wazazi na Familia,

Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb (DCSD) inathamini mawasiliano ya wazi na rahisi kati ya familia na shule na imejitolea kuhakikisha kuwa familia zote zinapata taarifa muhimu. Tungependa kukujulisha kuhusu huduma za ukalimani zinazopatikana kwako katika shule ya mtoto wako.


Huduma zifuatazo za lugha zinapatikana:

Huduma za Ukalimani Zinazotolewa na Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb	
<b>Huduma za Ukalimani wakati wa Mikutano</b>	DCSD hutoa wakalimani wakati wa mikutano. Ili kuomba mkalimani kwa mkutano ulioratibiwa, tafadhali wasiliana na shule ya mtoto wako kabla ya mkutano ili kuomba ukalimani.
<b>Ukalimani wa Simu ya Usaidizi ya DCSD</b>	Wafanyakazi wa shule wanaweza kupokea mawasiliano ya Simu ya Usaidizi ya DCSD (iliyoko katika Kituo cha Uchunguzi wa Wanafunzi wa Kimataifa) kwa simu fupi, zisizoratibiwa au za dharura.
<b>Ukalimani Kupitia Simu</b>	DCSD hutumia Programu ya ELSA Lite, Simu ya Waya ya ELSA, na Language Line Solutions ili kutoa ufikiaji wa mkalimani wa moja kwa moja kupitia simu katika zaidi ya lugha 240.
<b>Ukalimani wa Upande Mmoja/ Kupigiwa Simu</b>	Ikiwa mwalimu au mfanyakazi wa shule anahitaji kuwasiliana nawe ili kukupa taarifa fupi au ambazo hazijaratibiwa, anaweza kuomba mkalimani amsaidie kupiga simu nyumbani.
<b>Mawasiliano na Mwalimu</b>	Walimu hutumia programu mbalimbali ambazo hutoa mawasiliano ya kila siku kwa wazazi na familia. Nyingi za programu hizi huwa na uwezo wa kutafsiri ujumbe. Tafadhali wasiliana na mwalimu wa mtoto wako kwa maelezo zaidi.

Tunaamini kuwa mawasiliano madhubuti ndiyo ufunguo wa mafanikio ya mtoto wako na tunakuhimiza utumie huduma hizi ili kuhakikisha kuwa una taarifa kamili kuhusu elimu ya mtoto wako.

Ikiwa unahitaji usaidizi/maelekezo zaidi kuhusu mambo zaidi ya shule, tafadhali wasiliana na Idara ya Wanafunzi wa Kiingereza kupitia **(678) 676-6602**.

**Tafadhali kata sehemu iliyo hapa chini na uilete katika shule ya mtoto wako ili kuomba mkalimani:**



**LANGUAGE ASSISTANCE NEEDED**

**English Learners Department**

**HELLO!** I am a parent/guardian of a DeKalb County School District student and I speak \_\_\_\_\_.

I need assistance in my native language.

**PARENTS OR STAFF:** If you have any questions, please call the Interpretation and Translation Unit at **678-676-6602**.